

Mradi Namba 6505: KUFUNGA MTAMBO MPYA WA KISASA WA UCHAPAJI

Katika mwaka wa fedha 2022/23 kiasi cha **Sh. 9,400,940,000** fedha za ndani ziliombwa kwa ajili ya kuwezesha ufungaji wa mtambo tajwa. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mradi huu ni:

- (i) Kufunga mtambo mpya na wa kisasa wa uchapaji ambao utakuwa ni chanzo kikubwa cha mapato ya Kampuni.

Hadi kufikia tarehe **31 Disemba, 2022** Wizara ilipokea jumla ya kiasi cha **Sh. 809,591,776.59** sawa na **asilimia 8.6** ya bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Mradi tajwa. Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi husika ni kama ifuatavyo: -

- (i) Taratibu za manunuzi ya mitambo zimeshakamilika, mkataba ulishasainiwa na uzalishaji wa mashine unaendelea. Awamu ya kwanza ya mashine tisa (9) zimeshawasili Dar es Salaam na taratibu za kuzigomboa zinaendelea. Maombi ya kiasi cha Sh. bilioni 11.7 kwa ajili ya malipo ya mashine hizo tisa (9) yaliwasilishwa Hazina tarehe 16 Januari, 2023 baada ya kupokea nyaraka za madai kutoka kwa mzabuni na uthibitisho wa mashine kufika Dar es Salaam kutoka Benki. Ufuatiliaji wa karibu unafanyika. Kwa mujibu wa mkataba, Mkandarasi atalipwa baada ya uthibitisho wa mashine kusafirishwa na kufika bandari ya Dar es Salaam. Mashine nyingine tatu (3) ziko njiani na zinatarajiwa kuwasili nchini kati kati ya mwezi Februari, 2023.
- (ii) Taratibu za ujenzi zinakamilishwa na mkandarasi anatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi Januari, 2023 na kazi ya ujenzi kuanza mara baada ya mikataba husika kukamilishwa.
- (iii) Vibali kwa ajili ya ununuzi wa magari saba (7) vimepatikana kutoka ofisi ya Waziri Mkuu. Utaratibu wa ununuzi wa magari hayo unaendelea kupitia GPSA. Hata hivyo Kampuni inahitaji magari 34 kwa ajili ya shughuli zake za Makao Mkuu na Mikoani. Mahitaji haya yamewekwa kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/24.
- (iv) Taratibu za upatikanaji wa malighafi za uchapaji zimeanza kwa kutangaza zabuni.